

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**IJUMAA KAREEM KUTOKA KWA MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM.**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Paul C. Makonda leo amekutana na Masheikh na Viongozi wa Misikiti zaidi ya **Mia Sita (600)** ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Hatua hii ni muendelezo wa Mikutano yake na Makundi ya watu mbalimbali, katika kuuenzi Mwezi wa Mfungo wa Ramadhani.

Vilevile Mhe. Makonda ametoa vitu mbalimbali kama **SADAKA KWA KILA KIONGOZI** kwa kila Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam ambavyo ni:-

- 1. Mchele kg 25**
- 2. Ngano kg 25**
- 3. Sukari kg 25**
- 4. Mafuta ya kupikia lita 20**

Akizungumza na Masheikh na Viongozi wa Dini ya KIISLAMU, Mhe. Makonda ameanza kwa kuwapongeza kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali pamoja na kumuunga mkono Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi ambavyo anatekeleza utendaji wake wa kazi kwa kuhakikisha anaipoleka Tanzania kwenye nchi ya Uchumi wa kipato cha kati kupitia **MAPINDUZI YA VIWANDA.**

Mhe. Makonda pia amewaomba viongozi wa Dini kuutumia mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani kuhubiri **AMANI, UTULIVU NA KUVUMILIANA** katika kila mambo wanayoyafanya waumini wao.

Katika hatua nyingine, Mhe. Makonda amefanikiwa **KUWASHAWISHI** wafanyabiashara haswa wa **SUPERMARKET** Mkoa wa Dar es Salaam kufanya kazi mpaka saa sita za usiku, ili kutoa fursa kwa wananchi kujipatia mahitaji yao muhimu kipindi hiki cha **Mfungo wa Ramadhani.**

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

16/06/2017